BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 23 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Ripoti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

93. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

Sheria Namba 9 ya mwaka 2020 na Zanzibar Decree (Cap. 163) ya mwaka 1928 (kama ilivyokuwa ikitumika), zimeweka umbali usiopungua kilomita moja (1km) kutoka makaazi ya watu na sehemu za kijamii hadi sehemu za starehe zinazoambatana na ulevi. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa agizo hili limekuwa halifuatwi ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba.

Je, ni ipi kauli na hatua za Serikali kuhusiana na sehemu za starehe katika maeneo yaliyo karibu na makaazi ya watu kinyume na Sheria hii.

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

107. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ni jambo jema kwamba Serikali, baada ya uchunguzi wake wa kina, imeamua kuvikodisha visiwa 10 kati ya 53 vilivyopo Zanzibar kwa majaribio.

(a) Je, ni vipimo vipi na muda upi wa majaribio hayo.

(b) Kwa nini Serikali haiendelei kuvikodisha visiwa vingi zaidi na hasa ikizingatiwa kuwa, ukodishwaji huo ni baada ya kufanya uchunguzi wa kina na wa kitaalamu.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

98. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa siku za karibuni, Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekuwa zikifungua zaidi akaunti zake katika Benki nyengine isiyokuwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

(a) Je, ni kwa sababu gani Serikali imeziruhusu Taasisi zake kufanya hivyo.

(b) Je, Serikali haioni kwamba kufanya hivyo ni mwanzo wa kuidhoofisha PBZ.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

75. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika uwanja wa ndege wa Zanzibar eneo la Terminal II madereva wanaoingia na gari kupitia eneo lililotengwa kwa ajili hiyo, hulazimika kuingia na gari zao na kubonyeza kitufe ili gari iweze kuingia katika eneo hilo. Kwa vile mashine hizo zinatumia umeme na kuna siku umeme huzimika na kunapelekea ulazima wa kubadilisha utaratibu mbadala.

(a) Je, kwa kiasi gani jambo hili huathiri ukusanyaji wa mapato yatokanayo na matumizi ya umeme tu katika mashine hizo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka nishati mbadala (standby generator au solar panel) kwa ajili ya kuendesha mashine hizo ili kuondoa tatizo hilo.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

9. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAKA KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii ambayo inashiriki kikamilifu katika harakati za michezo. Na kwa kuwa Serikali kupitia Wizara hii ndiyo yenye dhamana na jukumu la kusimamia michezo kwa Zanzibar.

(a) Je, kupitia bajeti ya mwaka 2022/2023, Serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa lengo la kuinua michezo kwa watu wenye ulemavu.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha viwanja vya michezo vinavyojengwa vinakuwa jumuishi, ili watu wenye ulemavu waweze kufaidi matunda ya Serikali yao.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

157. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tunaipongeza Serikali kwa jitihada ya kuhudumia wananchi kwa kuwapatia mahitaji yao mbali mbali ikiwa ni pamoja na huduma ya maji safi na salama. Hata hivyo, kwa muda mrefu sasa, wananchi wa Bumbwisudi na Kinumoshi hawapati maji kutokana na kuharibika kwa mashine katika visima vya vijiji hivyo.

Je, ni lini tatizo hilo litaisha.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

6. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAKA KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu zake zote za uongozi, kwa kuimarisha Sekta ya Mifugo hapa nchini, ikiwa ni pamoja na upandishaji wa ng'ombe na uimarishaji wa mifugo kwa ujumla. Pamoja na juhudi zake hizo, kuna changamoto mbali mbali zinazoikabili mifugo hapa nchini.

(a) Je, kuna vituo vingapi vya upandishaji wa ng'ombe vilivyoimarishwa hapa nchini hadi sasa.

(b) Je, uzalishaji wa ng'ombe kutokana na kupandishiwa ukoje hivi sasa hapa nchini.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

146. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Kwa kuwa Serikali imekuja na mkakati wa kuimarisha viwanda vilivyopo na pia kuanzisha viwanda vipya nchini.

Je, ni ipi hali ya kiwanda cha Makonyo cha Wawi.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ripoti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Uchumi kwa mwaka 2021/2022.

Zanzibar,
23 Septemba, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.